**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAADILI NA HAKI ZA BINADAMU VIWANJA VYA NYERERE SQUARE JIJINI DODOMA**
**TAREHE 10 DESEMBA, 2023**

**SALAMU**

- ***Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;***

- ***Mheshimiwa Dkt. Balozi Pindi Chana (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria;***

- ***Comrade Anamringi Macha, Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi;***

- ***Mheshimiwa Prof. Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi;***

- ***Mheshimiwa Abdala Ulega (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi;***

- ***Mheshimiwa Anthony Mavunde (Mb), Waziri wa Madini;***

- ***Mheshimiwa Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;***

- ***Mheshimiwa Exaud Kigahe, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara;***

- ***Mheshimiwa Dustan Kitandula, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii;***

- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya wakiongozwa na Mheshimiwa Alhaji Shekimweri, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma;***

- ***Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu mkiongozwa na Ndugu Mululi Majula Mahendeka, Katibu Mkuu Ikulu;***

- ***Waheshimiwa Wabunge;***

- ***Bw. Charles Kicheere, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG);***

- ***Wakurugenzi, Mameneja, Viongozi na Watendaji wa Serikali na sekta binafsi;***

- ***Wawakilishi wa Mashirika ya Maendeleo;***

- ***Kamati za Usalama za Mkoa na Wilaya;***

- ***Viongozi wa Taasisi za Dini;***

- ***Viongozi wa Kimila wa kabila la Wagogo;***
- ***Ndugu Wananchi;***
- ***Wanahabari;***
- ***Mabibi na Mabwana;***
- ***Wasanii wetu wa Kwaya ya JKT na Kwaya ya TAKUKURU***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**UTANGULIZI**

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa,*** awali ya yote nimshukuru Mola wetu Mtukufu, mwingi wa rehema, kwa kuturuzuku uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana hapa kwa ajili ya kuhitimisha Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu kwa mwaka 2023.

**Pili**, ninawapongeza viongozi wa taasisi mbalimbali, Chama cha Mapinduzi, viongozi wa madhehebu ya dini na viongozi wa kimila mlioshiriki katika maadhimisho haya.

**Tatu,** ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri Mheshimiwa Dkt. Balozi Pindi Chana (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**Kipekee,** ninawapongeza wananchi wote wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mheshimiwa Rosemary Senyamule kwa kuthamini masuala ya maadili na haki za binadamu. Ushiriki wenu ni ishara ya dhamira ya pamoja ya Watanzania ya kuhakikisha kuwa uadilifu unajengwa, rushwa inadhibitiwa na haki za binadamu zinalindwa ipasavyo.

**LENGO LA MAADHIMISHO**

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa,*** nimeelezwa kuwa maadhimisho haya yamefanywa kwa lengo la kuadhimisha Kitaifa Mkataba wa Kimataifa wa Mapambano dhidi ya Rushwa pamoja na Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu. Aidha, katika maadhimisho haya leo, nitatoa vyeti kwa taasisi zilizoshiriki katika kutoa huduma kwa umma ili kutambua mchango mkubwa zinazoutoa kwa umma wa Watanzania katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

**SALAMU ZA VIONGOZI WAKUU WA NCHI**

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipaswa kuwa mgeni rasmi katika

kilele cha maadhimisho haya lakini kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa imempendeza nimuwakilishe. Pamoja na salamu kwa maadhimisho haya amesisitiza umuhimu wa kila mmoja kuendelea kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa na vitendo vingine vya ukiukwaji wa haki za binadamu.

***Ndugu Wananchi,*** nimekuja pia salamu nyingi za heri kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**KAULIMBIU YA MAADHIMISHO**

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** maadhimisho ya mwaka huu yamebebwa na kaulimbiu isemayo "***Zingatia Maadili, Utu, Uhuru na Haki kwa Maendeleo Endelevu.*** Kaulimbiu hii inachagiza masuala ya msingi yanayohusu maendeleo endelevu kutokana na ukweli kwamba kizazi huru chenye uadilifu, utu na kinachozingatia haki ni msingi wa maendeleo ya Taifa lolote. Hivyo basi, hatuna budi wananchi wote kuunganisha nguvu katika ujenzi wa kizazi chenye misingi ya maadili.

Kaulimbiu hii kwa upande mwingine, ni wito kwa kila mmoja wetu, kwa nafasi yake, rika lake na jinsia yake kutekeleza wajibu wake katika ujenzi wa kizazi chenye maadili na hatimaye kujenga jamii yenye ustawi. Licha ya hayo, kaulimbiu hii ni wito kwa sekta ya umma na sekta binafsi kutimiza wajibu wake kuhusu masuala ya maadili, utu, uhuru na haki. Kwa maneno mengine kaulimbiu hii imegusa taasisi zote na inasisitiza uwajibikaji wa kila mmoja wetu. Ninawapongeza sana kwa kuja na kaulimbiu hii inayotukumbusha wajibu wetu kama jamii wa kuzingatia maadili, utu, uhuru na haki kwa maendeleo endelevu.

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** ni ukweli usiopingika kuwa maadili yanajengwa kuanzia kwenye taasisi ya msingi, taasisi ya kwanza ni familia. Taasisi ya pili ni shule, ambayo inawajibika kuweka mifumo ya kuendeleza kile kilichopatikana nyumbani. Kadhalika nyumba za ibada, tunategemea ziwe chachu ya kujenga maadili mema kwa misingi ya kiroho na hatimaye ushiriki wa jamii nzima kupitia wazee wa ukoo, jadi na wazee maarufu katika makuzi ya mtoto.

**UPEKEE WA MAADHIMISHO YA MWAKA 2023**

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** ninatambua kuwa maadhimisho ya mwaka huu yameenda sambamba na Maadhimisho ya Miaka 75 ya Tamko la Dunia Kuhusu Haki za Binadamu la mwaka 1948. Nchi yetu ni miongoni mwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa ambao ni chimbuko la mikataba mingi ya kimataifa na kikanda ambayo Tanzania imeridhia. Nchi yetu imepiga hatua kubwa katika kusimamia na kutekeleza masuala ya haki za binadamu na kuzingatia misingi ya utawala bora katika vipindi vya kabla na baada mwaka 1984 ambapo haki za msingi za binadamu ziliingizwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na ile ya Zanzibar ya mwaka 1984 (Toleo la 2010).

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** Awamu zote za Serikali zimekuwa zikilinda, zikitekeleza na kusimamia haki za binadamu nchini kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo katika Ibara ya 12 hadi 24 imebainisha Juu ya haki za binadamu. Lakini pia, ibara ya 25 hadi - 30 ya

Katiba hiyo imebainisha wajibu wa jamii na pia imeweka wazi majukumu ya mihimili mikuu mitatu ya nchi yetu ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama.

Aidha, Serikali imeanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, taasisi huru ya Kitaifa ya haki za binadamu yenye jukumu la Kikatiba na Kisheria la kuhamasisha hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia kuitekeleza.

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** kwa upande wa kukabiliana na dhuluma na rushwa, mnamo mwaka 1971, Sheria mama ya Kuzuia Rushwa nchini ilitungwa. Sheria hiyo ndio iliyozaa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007. Jitihada hizo zimeendelea na sasa nchi yetu inatekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa ambao hadi sasa umetekelezwa kwa awamu tatu.

***Aidha,*** nimefurahi kusikia kuwa tayari mkakati wa nne umeandaliwa na kwamba maandalizi yalishirikisha wadau wote muhimu. Jambo ambalo limenipa faraja kubwa katika mkakati wa nne ni kitendo cha kuainisha majukumu ya wadau wote nchini. Niwahimize wadau wa sekta binafsi, asasi za kiraia, wanahabari, taasisi za dini, na washirika wa maendeleo endeleeni kusimamia maeneo yao ya kiutendaji.

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali inawajibika kuimarisha ustawi wa Wananchi. Katika kutekeleza jukumu hilo la Kikatiba, Serikali imeendelea kuhakikisha inajenga uchumi imara wa mtu mmoja mmoja na uchumi wa Taifa. Aidha, inajenga uhusiano mzuri baina ya makundi yote yaliyomo nchini sambamba na kuwahakikishia wananchi uwepo wa utulivu, amani na huduma bora zinazokidhi matarajio yao.

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** jitihada zote hizo za Serikali zitakuwa na matokeo chanya ikiwa jamii nzima itanufaika na kuwajibika katika kuhakikisha kuwa miundombinu inayojengwa inaendelea kuwa salama na huduma zinatolewa kwa maslahi mapana ya umma wa Watanzania badala ya watu vikundi vya watu wachache. Hii ni sababu iliyotia msukumo kwa Serikali kuweka vyombo mbalimbali vya usimamizi wa masuala ya Maadili, Haki za Binadamu na Kuzuia Rushwa nchini.

Hata hivyo, ufanisi wa utendaji kazi wa vyombo hivi unahitaji sana ushirikiano wa wananchi wanufaika wa huduma hizo. Wananchi tambueni kuwa mnalo jukumu la kufichua vitendo vya rushwa na vitendo vya ukosefu wa maadili. Watumiaji wa huduma watambue kuwa wanalo jukumu la kufichua vitendo vya ukosefu wa maadili, uvunjifu wa haki za binadamu na vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya watoa huduma katika sehemu mbalimbali.

## UZINDUZI WA AWAMU YA NNE YA MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** kama nilivyotangulia kusema tayari Serikali imeshaandaa Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa ambao katika Maadhimisho haya nitauzindua rasmi na kugawa nakala kwa baadhi ya wawakilishi wa makundi yaliyopo. Mkakati huu umezingatia wajibu wa wadau wote nchini kuanzia wananchi, Taasisi za Serikali; taasisi zisizo za Serikali ikijumuisha sekta

binafsi, asasi za kiraia, mashirika yasiyo ya Serikali, taasisi za dini, washirika wa maendeleo, wanahabari na vyama vya siasa.

Licha ya hayo, elimu kuhusu mkakati huo imeshaanza kutolewa na itaendelea kutolewa ili kuwezesha wadau wote kuwa na uelewa wa pamoja na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mkakati.

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** mmomonyoko wa maadili katika jamii una athari kubwa kwa misingi ya utawala bora ambayo miongoni mwake ni uadilifu na udhibiti wa rushwa. Misingi hii ikitetereka inaathiri juhudi za kuleta maendeleo nchini. Hivyo basi, taasisi zote za kijamii ikianzia familia, dini na shule ziendelee kuhimiza maadili mema, ili kila mmoja ashiriki kujenga utamaduni wa uwajibikaji na hatimaye kuwa na utendaji wa kiadilifu.

**WAJIBU WA WANANCHI KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA**

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 katika Ibara ya 8(1)(a) imeweka bayana kuwa **rushwa ni adui wa haki**. Hivyo, imetoa maelekezo kwa Serikali kuimarisha mifumo na mamlaka ya kuzuia na kupambana na rushwa nchini yaani TAKUKURU ili iweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi. Shughuli hizo ni pamoja na kukabili vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali, kudhibiti matumizi mabaya ya ofisi na upotevu wa fedha za umma. Shughuli nyingine ni kubuni na kutekeleza mikakati mipya ya kupambana na rushwa na ufisadi pamoja na kufanya tafiti ili kubaini na kuziba mianya mipya ya rushwa na ufisadi. Vilevile, kuhamasisha ushiriki wa jamii na kutoa elimu katika mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi.

Suala la ushiriki wa jamii ni la msingi kwa kuwa wananchi ni wadau muhimu sana katika utekelezaji wa Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa. Jamii ina jukumu la msingi katika kuzuia vitendo vya rushwa kabla havijafanyika kwa kukataa kutoa ama kupokea rushwa na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa. Ninyi ni wadau wakubwa wa kukomesha rushwa na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu. Ili nchi yetu isiwe na ukiukwaji wa haki za binadamu, wananchi mnapaswa kufichua vitendo vya ukosefu wa maadili na uvunjifu wa haki za binadamu.

Mtanzania usikubali kutoa rushwa popote, hasa kwenye maeneo unayopaswa kupewa huduma hiyo. Wewe ni Mtanzania unalindwa na sheria za nchi za kupata huduma bure kama vile hospitali bila kutoa rushwa. Inatakiwa kila Mtanzania abebe jukumu hili kwa mikono miwili, alisimamie na alitekeleze.

Upo usemi usemao ***Kinga ni bora kuliko tiba***, katika mazingira haya usemi huu ni halisi kwani ni ukweli usiopingika kuwa juhudi nzuri katika mapambano dhidi ya rushwa ni za kuzuia kuliko kusubiri madhara yatokee na kuanza kupambana.

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** rushwa wakati wote ni adui wa haki, Serikali inapinga rushwa na vitabu vya dini vinapinga rushwa. Ninaomba ninukuu maandiko katika Qur'aan Tukufu Sura ya 2 Aya ya 188 "**Wala msiliane mali zenu kwa batili (kinyume cha haki) na kuzipeleka kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali ya watu kwa dhambi, na hali mnajua."**

Biblia Takatifu katika kitabu chake kutoka Sura ya 23 mstari wa nane nayo inakemea rushwa. Ninaomba kunukuu "**nawe usipokee rushwa; kwani rushwa hupofusha macho hao waonao".**

Nukuu hizo zinaonesha kuwa rushwa inakatazwa katika vitabu vya imani zote na kwa kuwa Watanzania ni watu wa imani tunawahitaji sana katika kutokomeza rushwa hapa nchini. Sote tushirikiane katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kukataa kutoa na kupokea rushwa.

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** pamoja na dhamira ya dhati ya Serikali katika kuzuia maovu ndani ya jamii yetu hususan rushwa, pasipo ushirikiano na wadau wote muhimu wakiwemo wananchi, haitaweza kushinda mapambano hayo kwa kuwa vitendo vya rushwa aghalabu hufanywa kwa siri. Serikali kwa kutambua hilo, kupitia utekelezaji wa Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa itatoa elimu ya maadili na kuzuia vitendo vya rushwa kwa kushirikiana wa karibu na wadau wote.

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** nimeelezwa kuwa mkakati ulioandaliwa unao mpango madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini ambao umesheheni viashiria vitakavyosaidia katika kupima utekelezaji. Kupitia mpango huo, kila taasisi inaweza kujipima na kubaini kama inatekeleza Mkakati huo ipasavyo. Nitoe rai kwa taasisi kufanya ufauatiliaji ili kuona hali halisi ya utekelezaji wa mkakati, kubaini vikwazo vilivyopo na kufanya maboresho pale inapohitajika.

**MAENEO YA MSISITIZO**

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** sambamba na maelezo yangu ninapenda kutumia hafla hii kutoa msisitizo katika msuala machache yafuatayo;

**MOSI:** Uandaliwe mpango mahsusi wa kuelimisha umma kuhusu Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa. Tumieni pia watu mashuhuri na redio za kijamii ili umma ufahamu wajibu wao kama ulivyobainishwa na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake.

**PILI:** Vyama vya Jamii ya watu wenye ulemavu vishirikishwe katika mpango wa mafunzo kuhusu Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa.

**TATU:** Wananchi wote mjitokeze kushiriki kikamilifu kwenye mafunzo au mikutano inayohusu elimu kuhusu Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa. Wakati ukifika shime mshiriki ili kupata uelewa wa kutosha wa Mkakati na kutekeleza ipasavyo ili kudhibiti rushwa nchini.

**NNE:** Wananchi wote wazingatie kuwa watumishi wa umma na wa sekta binafsi ambao wanatoa huduma kwa wananchi wanapata mishahara yao na hawapaswi kupewa malipo kwa huduma wanazozitoa.

**TANO:** Sekta zote nchini ziwajibike kuweka wazi na kutoa elimu kuhusu malipo ambayo wateja wao wanapaswa kuyalipa. Uwazi katika kutoa huduma uanzie ndani ya taasisi na kuwekewa msisitizo maalum kwa wateja na wananchi kwa ujumla.

**SITA:** Watumishi wote wa sekta ya umma na binafsi wafanye kazi kwa kuzingatia misingi ya utu na haki za binadamu wanapohudumia wananchi. Suala hili litawezekana endapo kila taasisi itazingatia maadili na haki za binadamu wakati wote.

**SABA:** Viongozi wa madhehebu yote ya dini endeleeni kukaripia vitendo vya rushwa. Serikali inatambua viongozi mmekuwa wakati wote mkiisaidia Serikali katika masuala mbalimbali, ninawasihi msichoke, endeleeni kupaza sauti zenu kwa kuwafundisha waumini wenu kuacha vitendo vya rushwa, uvunjifu wa haki za binadamu na vitendo vyote kinyume na maadili.

**NANE:** Wadau wote watakaoshirki katika kutekeleza Afua za kuzuia rushwa katika maeneo ya kiutendaji msisite kujifunza kupitia uzoefu kwa Taasisi za Serikali ambazo zilitekeleza kikamilifu Mkakati katika awamu ya kwanza, ya pili na awamu ya tatu.

**TISA:** Ulinzi wa Haki za Binadamu unahitaji uadilifu mkubwa wa jamii. Hivyo basi, watoa huduma kwa wananchi hususan Watumishi wa Umma ongezeni viwango vya juu vya uadilifu mnapotoa huduma kwa wananchi.

**KUMI:** Rushwa ni zao la uvunjifu wa maadili ambalo husababisha haki mbalimbali za binadamu kukiukwa. Kila mwananchi atimize wajibu kukataa rushwa kwa vitendo. Ewe mwananchi usikubali kununua haki yako kwa namna yoyote.

**KUTAMBUA MCHANGO WA WADAU**

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** nimejulishwa kuwa maandalizi ya Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa yamefanikiwa kutokana na ushirikiano na juhudi za pamoja baina ya Serikali na Wabia wa Maendeleo (FCDO) kupitia Mradi wa BSAAT na UNDP ambao kwa nyakati tofauti waliwezesha maandalizi haya.

Kipekee ninawashukuru wabia wetu wa maendeleo wa FCDO na UNDP kwa kuchangia jitihada za Serikali za kukabili vitendo vya rushwa nchini. Niwahakikishie kuwa Serikali yetu iko tayari kuendeleza ushirikiano nanyi ili hatimaye Mkakati ulioandaliwa utekelezwe kwa ukamilifu. Kadhalika, nitumie fursa hii kuwakaribisha washirika wengine wenye utayari waje kuungana na Serikali katika utekelezaji wa Mkakati huu.

***Ndugu Wananchi na wageni waalikwa;*** sote tumemsikia Mheshimiwa Boniface Simbachawene (Mb.) Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika maelezo yake akitaja Mshauri Elekezi “ESRF na wataalamu wetu  ambao ni Watumishi wa Serikali kuwa ndio walioandaa Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa nitakaozindua leo hivi punde. Nitumie nafasi hii kuwapongeza sana kwa kazi nzuri walioyoifanya.

Ninawapongeza Kamati ya Maandalizi pamoja na  wadau wote walioshiriki kuandaa maadhimisho haya ambayo kwa hakika yamekidhi malengo yaliyokusudiwa.

Ninawapongeza pia wananchi wote ambao wamekuwa wakijitokeza katika viwanja hivi na kupata huduma mbalimbali. Ninatambua pia uwepo wa taasisi 20 zilizokuwa zikitoa huduma ikiwemo ya elimu kwa wananchi waliokuwa wakifika katika viwanja hivi vya Nyerere Square. Ninatoa pongezi nyingi kwa watendaji na wataalam wote waliofanya kazi kubwa ya kuwahudumia wananchi. Ninaamini uwepo wenu katika viwanja hivi umekuwa wa manufaa sana kwa watu wote waliofika mahali hapa.

**HITIMISHO**

**Ndugu Wananchi,** nimalizie kwa kuwashukuru sana wananchi pamoja na wadau wote kwa kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuhakikisha jamii yetu inaishi katika misingi ya uadilifu. Niwatakie utekelezaji mwema wa Mkakati huu shirikishi kwa jamii nzima.

Baada ya kusema haya sasa niko tayari kuzindua rasmi **Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa** na kutoa vyeti **kwa taasisi zilizoshiriki katika kutoa huduma kwa umma katika viwanja hivi kwa siku tano** na sasa ninatamka kuwa **Maadhimisho ya Kitaifa ya Mkataba wa Kimataifa wa Mapambano Dhidi ya Rushwa Pamoja na Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu kwa mwaka 2023 yamefungwa rasmi.**

**MUNGU IBARAKI TANZANIA!**
**MUNGU IBARIKI AFRIKA!**
**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA.**